## HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

### UTARATIBU WA KUTOA LESENI

**LESENI YA BIASHARA**

Hiki ni kibali maalum cha Serikali kinachotolewa kwa mfanyabiashara yeyote anapotaka kufanya biashara hapa nchini. Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya 1972 – Kifungu cha 3(a) kimeweka bayana kuwa, Kibali hicho maalumu kinaitwa Leseni ya Biashara. Kwa hiyo basi, kufanya biashara yoyote bila kuwa na kibali hiki ni kosa la jinai.

**UTARATIBU ZA UTOAJI WA LESENI ZA BIASHARA KATIKA HALMASHAURI YA MUFINDI**

Mtu yeyote raia wa Tanzania anayo haki ya kupatiwa leseni ya biashara ili mradi awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18) Mwenye akili timamu ambaye hajawahi kupatikana na kosa la jinai na awe na eneo la kufanyia biashara kisheria. Maelezo ya awali ya namna ya kuomba na matumizi ya leseni:

1. Jaza fomu 2 za maombi ya Leseni (TFN 211) kwa kundi A inapatikana ofisi ya Biashara
2. Soma kwa makini na jaza kila kipengele kwenye fomu ambacho kinahusiana na biashara yako. Ni muhimu kusoma maelezo yote yaliyoko kwenye fomu kabla hujaondoka ofisi ya Biashara ili uweze kupata maelekezo kwenye vipengele ambavyo hujavielewa.
3. Ukaguzi wa maafisa Mipango miji, Afya na Biashara utafanyika katika eneo Biashara inayokusudiwa kufanyika mfano: Bucha, nyumba za kulala wageni, miga hawa, stoo za mkaa, gereji, mashine za kusaga na kukoboa nafaka.(Maafisa hawa takagua na kutoa ushauri kulinga na aina ya biashara, eneo lilochaguliwa kwa ajili ya biashara kama ni eneo linalotumika kwa biashara husika,
4. Baada ya kukamilisha mchakato, muombaji atatakiwa kuwasilisha fomu ya maombi iliyoidhinishwa na Mamlaka ya MapatoTanzania kwa ajili ya kufanyiwa makadirio ya kodi (mabadiliko ya ulipaji kodi ya biashara baada ya siku 90 ya kuanza biashara)
5. Utoaji wa leseni
6. Muda wa leseni
7. Leseni za ushauri na utaalamu maalum pia hutolewa kwa ajili ya kutoa huduma ya ushauri na utaalamu ambapo mhusika ni lazima awe amesomea fani aliyoomba au kuajiri mtu mwenye sifa zinazotakiwa
8. 

| | Huduma | Utaalamu na Mamlaka husika |
|---|---|---|
| I. | Ukandarasi wa ujenzi | Bodi ya ukandarasi |
| II. | Utengenezaji wa mahesabu/ ukaguzi wa hesabu | Bodi ya wahasibu na wakaguzi |
| III. | Upuliziaji dawa za kuua wadudu kwenye mashamba na majengo | Tropical Pesticides Research Institute (TPRI) |
| IV. | Uwakili | Tanganyitika Law Society |
| V. | Udaktari | Medical Council of Tanzania |
| VI. | Uuzaji wa madawa, chakula na vipodozi | Tanzania Food & Drugs Authority |
| VII. | Uuzaji wa dawa za binadamu | Tanzania pharmacy council |
| VIII. | Uuzaji wa dawa za Mifugo na kilimo | Tanzania Veterinary Council |

9. Ni kosa kisheria kufanya biashara bila kuwa na leseni, adhabu yake ni kulipia shilingi 50,000 hadi 100,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote. Mtu yeyote atakayechelewa kuhuisha leseni yake baada ya siku 21 baada ya muda wa leseni kuisha atalipia asilimia 25 ya ada iliyotakiwa kulipia na itaongezeka asilimia 2 kila mwezi kadri mfanyabiashara anavyochelewa kuhuisha leseni ya biashara

**MASHARTI YA KUOMBA NA KUPEWA LESENI**

1. Mfanyabishara anapaswa awe na hati ya usajili iwapo anatumia jina la biashara (Certificate of Registration or Incorporate)
2. Kama ni Kampuni, muombaji awe na "Memorandum of Article of Association" ambazo zinaonyeesha kuwa kampuni imeruhusiwa kufanya biashara anayo iomba.
3. Awe na mahali/ eneo linalokubalika kwa aina ya biashara anayoioomba na isiwe vibanda vilivyopo kano kando ya biashara.
4. Mfanyabiashara aje na kivuli cha cheti kinachoonyesha kuwa amelipa mapato kwa mujibu wa Sheria (Tax clearance) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
5. Masharti mengine ya kupata leseni hutegemea aina ya biashara mtu anayotaka kuanzisha mfano mgahawa inabidi afuate taratibu zote za afya na kupima wafanyakazi wake.
6. Hati ya utaalamu(professional Certificates) kwa biashara ote za kitaalam.
7. Maombi ya leseni yasihusishwe na ulipaji wa michango au malipo mengine yoyote yasiyohusu sheria hii, isipokuwa ada ya leseni ya biashara,faini au adhabu pale inapohusika chini ya sheria hii.

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

### MUDA WA LESENI

1. Muda wa leseni ni miezi 12 tangu leseni inapolipiwa. Baada ya leseni kwisha muda wake wa kutumika, mfanyabiashara anapewa siku ishirini na moja (21) za kuhuisha leseni yake bila adhabu (penati), akichelewa atalipia na ada ya leseni pamoja na adhabu (penati) ambayo huanza kwa asilimia ishirini na tano (25%) na huenda ikiongezeka kwa asilimia mbili (2%) kila mwezi.
2. Leseni za kileo ni miezi 6 tangu leseni inapolipiwa.

### KUHUISHA LESENI YA MFANYABIASHARA

Mfanyabiashara anayehuisha leseni anatakiwa aje na nakala ya leseni inayoisha muda wake pamoja na kibali cha mlipa kodi (Tax Clearence Certificate) kutoka TRA na kupeleka moja kwa moja kwa Afisa biashara anayehusika.

### MASHARTI YA UTUMIAJI WA LESENI

Leseni za vileo zina masharti mengi ikiwa ni pamoja na kutouza kilevi kwa watoto . Masharti mengine ni muda wa kuuza pombe na kelele za muziki. Muda wa kuuza pombe ni kama ifuatavyo:-

### BAA (Retailers On licence)

| | | |
|---|---|---|
| (a) | Maeneo ya mjini: | |
| | Jumatatu hadi Ijumaa | - Saa 10.00 jioni hadi saa 5.00 usiku. |
| | Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu | - Saa 10.00 asubuhi hadi saa 6.00 usiku. |
| | | |
| (b) | Maeneo ya vijijini: | |
| | Jumatatu hadi Ijumaa | - Saa 10.00 alasiri hadi saa 2.00 usiku. |
| | Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu | - Saa 10.00 mchana hadi saa 5.00 usiku. |
| | Aidha inazingatia sheria ndogo ya Kijiji husika | |

### POMBE ZA ASILI (Local Liquour Licence)

| | | |
|---|---|---|
| | Jumatatu hadi Ijumaa | - Saa 10.00 mchana hadi saa 2.usiku. |
| | Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu | - Saa 10.00 asubuhi hadi saa 5.00 usiku. |
| | Inazingatia sheria ndogo ya Kijiji husika | |

Mfanyabiashara yeyote wa pombe anapaswa kufuata utaratibu huu ambao ni wa kisheria.

### MAKOSA

1. Kuendesha biashara bila leseni
2. Kuendesha biashara eneo tofauti na linaloonyeshwa kwenye Leseni.
3. Kutumia leseni moja kufanya biashara zaidi ya moja au maeneo mawili au zaidi na Serikali.
5. Kutokuweka leseni ya biashara mahali ambapo inaonekana kwa urahisi (Kuficha leseni).
6. Kutoa maelezo ya uongo ili kupata leseni au kukwepa kulipa ada /kodi inayostahili
7. Kumzuia Afisa wa Serikali aliyepewa mamlaka ya kukagua kufanya kazi yake.

### WAJIBU WA MFANYABIASHARA

1. Kulipia leseni ya biashara yake kwa mujibu wa makadirio kila mwaka au baada ya miezi 6
2. Ni jukumu la kila mfanyabiashara kumiliki leseni katika eneo lake la biashara na kuiweka mahala pa wazi ili kuonekana kwa urahisi

### FAIDA ZA MFANYABIASHARA KUWA NA LESENI NI PAMOJA NA;

1. Kutambulika kama mfanyabiashara halali
2. Husaidia kupata mikopo mbalimbali
3. Husaidia kupata fursa mbalimbali za kibiashara
4. Kuchangia katika Uchumi wa Taifa
5. Kuepuka usumbufu wa kufungiwa biashara kwa kutokuwa na leseni halali kwa mujibu wa sheria.

USAID KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI
VEGA Volunteers for Economic Growth Alliance
iesc THE NONPROFIT THAT MEANS BUSINESS

FEED THE FUTURE
The U.S. Government's Global Hunger & Food Security Initiative

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

| NA. | AINA YA BIASHARA | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1. | Maduka ya rejareja | 50,000 |
| 2. | Mashine za kusaga na kukoboa | 30,000 |
| 3. | Ukamuaji wa mafuta | 30,000 |
| 4. | Kiosk | 40,000 |
| 5. | Guest House | 80,000 |
| 6. | Glocery | 40,000 |
| 7. | Mpesa | 50,000 |
| 8. | Maduka ya madawa muhimu | 100,000 |
| 9. | Maduka ya vifaa vya ujenzi/hardware | 150,000 |
| 10. | Maduka ya vifaa vya umeme na vifaa vya nyumbani | 100,000 |
| 11. | Stationary/bookshops | 80,000 |
| 12. | Biashara ya Mbao | 100,000 |
| 13. | Ushonaji | 30,000 |
| 14. | Studio | 50,000 |
| 15. | Saluni za kike/kiume | 20,000 |
| 16. | Tea room/mgahawa | 25,000 |
| 17. | Mitumba | 15,000 |
| 18. | Maduka ya nguo mpya | 80,000 |
| 19 | Uselemala | 60,000 |
| 20. | Welding | 50,000 |
| 21. | Vifaa vya gari | 130,000 |
| 22. | Vifaa vya Baiskeli | 30,000 |
| 23. | Maduka ya Urembo | 50,000 |
| 24. | Usafirishaji | 200,000 |
| 25. | Ukandarasi wa umeme | Class D: 100,000 |
| | | Class A: 500,000 |
| 26. | Hosteli | 80,000 |
| 27. | Shule za msingi binafsi | 300,000 |
| 28. | Shule za sekondari binafsi | 500,000 |
| 29. | Vyuo vya binafsi | 500,000 |
| 30. | Logging | 100,000 |
| 31. | Vifaa vya simu | 50,000 |
| 32. | Vifaa vya pikipiki | 80,000 |
| 33. | Maduka ya jumla | 150,000 – 200,000 |
| 34. | Maduka ya vyombo vya nyumbani | 100,000 |
| 35. | Gereji | 120,000 |
| 36. | Butcher | 60,000 |
| 37. | Kusaga na kufungasha nafaka | 80,000 |
| 38. | Karakana | 60000 |
| 39. | Maduka ya pembejeo za kilimo | 60,000 |
| 40. | Vituo vya Mafuta | 150,000 |
| 41. | Vyama vya kuweka na kukopa | 200,000 |
| 42. | Mushroom | 80,000 |
| 43. | Kiwanda kidogo | 400,000 |
| 44. | Kiosk/Glocery ndogo vijijini | 10,000 |
| 45. | Biashara nyinginezo | 50,000 |

**IMEANDALIWA NA:**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MUFINDI

USAID KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

VEGA Volunteers for Economic Growth Alliance

iesc THE NONPROFIT THAT MEANS BUSINESS